TANGAZO LA SERIKALI Na. 31 la Tarehe 17/1/2025

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA), (SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153(1))*

## MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA USAFI, AFYA NA HIFADHI YA MAZINGIRA YA HALMASHAURI YA WILAYA YA ARUSHA YA MWAKA 2025

Jina

TS. Na. 921 la 2023

**1.** Sheria Ndogo hii itajulikana kama Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Usafi, Afya na Hifadhi ya Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Arusha ya Mwaka 2025, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Usafi, Afya na Hifadhi ya Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Arusha ya Mwaka 2023 ambayo katika Sheria Ndogo hii inarejewa kama "Sheria Ndogo kuu".

Marekebisho ya aya ya 3

**2.** Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika aya ya 3 kwa kufuta na kuandika upya tafsiri ya msamiati "taka ngumu" kama ifuatavyo:

> ""taka ngumu" maana yake ni vitu ambavyo si vya majimaji vitokanavyo na shughuli za majumbani, mitaani, biashara, viwandani na kilimo na inajumuisha takataka au taka za vyakula, vitu ambavyo si vya majimaji vitokanavyo na shughuli za ujenzi na ubomoaji, ufyekaji bustani na shughuli za madini, mizoga na mabaki ya magari mabovu;".

Marekebisho ya aya ya 8

**3**. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa kwa kufuta na kuiandika upya aya ya 8 kama ifuatavyo:

"Choo cha watu wenye mahitaji maalumu

**8.** Mtu yeyote anayetaka kujenga choo cha watu wenye mahitaji maalumu atahakikisha kwamba choo atakachojenga kinakuwa na maji, sakafu inayosafishika, banda imara la kudumu lililoezekwa na lenye mlango imara, bomba la kutolea hewa chafu na lenye mfuniko kwenye tundu la choo na shimo salama na safi kwa ajili ya kutupa kinyesi na mkojo wa binadamu, lililojengwa kwa vifaa vya kudumu, miundombinu ya watu wenye mahitaji maalumu na kuwa safi wakati wote.".

Marekebisho ya aya ya 11

**4.** Sheria Ndogo kuu inarekebishwa kwa kufuta aya ya 11(4).

Marekebisho ya aya ya 25

**5.** Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika aya ya 25 kwa kufuta na kuandika upya aya ndogo ya (6) kama ifuatavyo:

"(6) Kabla ya kuuza mfugo chini ya aya ndogo ya (5), Mkurugenzi atatoa taarifa ya siku saba kwa mmiliki na umma kuhusu kusudio la kuuza mfugo huo.".

Marekebisho ya aya ya 26

**6.** Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika aya ya 26 kwa -

(a) kuifanya aya ndogo ya (1) kuwa aya ya 26; na

(b) kufuta aya ndogo ya (2).

Marekebisho ya Jedwali la Nne

**7.** Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kichwa cha habari cha Jedwali la Nne kwa kufuta neno "USAJILI,".

Dodoma,
25 Machi, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri Wa Nchi- OR-TAMISEMI*